JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA NNE Aprili 2024



## Rais Samia atoa tani 189 za mbegu-Waziri Mkuu

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA

www.pmo.go.tz

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema kuwa Rais Dkt. Samia ameridhia kutoa tani 189 za mbegu za mpunga, mahindi na alizeti ili zisambazwe kwa wakulima wa wilaya ya Kilombero.

"Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anatoa pole kwa wananchi wote walioathirika na mafuriko yaliyotokana na mvua zinazonyesha nchini, lakini pia ametoa mbegu hizo ili kuhakikisha wale waliopata athari katika mashamba yao waweze kuendelea na shughuli za kilimo pale hali itakapokaa sawa," amesema.

Ameyasema hayo leo wakati akizungumza na wananchi wa maeneo ya Mlimba, Taweta, Masagati wilayani Kilombero, mkoani Morogoro ambako alikwenda kukagua athari za mafuriko.

Waziri Mkuu ambaye pia alikagua bonde la mto Kilombero linalojumuisha wilaya tatu za Kilombero, Ulanga na Malinyi, amesema Rais Samia ameelekeza Serikali iendelee kuwahudumia wananchi wote waliopata athari ikiwemo kuimarisha maeneo ya utoaji huduma za afya, kugawa vyakula na kurejesha miundombinu ikiwemo barabara na reli.

"Watanzania tuwe watulivu, Serikali yenu ipo kazini. Rais wetu Dkt. Samia ametupa maelekezo ya kuhakikisha tunawahudumia na kurejesha hali, tutaleta vyakula na tayari madaktari takribani 20 wameshasambazwa kwenye mikoa ya Morogoro na Pwani ili waweke kambi za utoaji huduma za afya."

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameziagiza TARURA, TANROADS na TAZARA zishirikiane kufanya ukarabati katika maeneo yote yaliyopata athari wakati Serikali inasubiri kumalizika kwa mvua ili iweze kufanya ukarabati mkubwa.

Waziri Mkuu anaelekea Ikwiriri, Muhoro na Chumbi wilayani Rufiji, mkoani Pwani ambako atakagua athari za mafuriko na kuwasalimia wananchi.

# Waziri Mkuu akagua athari za maafa Rufiji




WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amewataka wananchi waliokumbwa na adha ya mafuriko nchini waendelee kuwa watulivu wakati Serikali ikiendelea kuratibu utoaji wa misaada kwenye maeneo yaliyoathirika.

"Barabara ya Mkongo hadi Utete na ile ya kutoka Mloka Mkongo zote zimeathirika. Tunafanya kazi ya kurejesha mawasiliano ili wananchi waweze kupata huduma muhimu," amesema.

Waziri Mkuu ametoa wito huo leo jioni wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Chumbi, wilayani Rufiji, mkoani Pwani ambako alikwenda kukagua athari za mafuriko kwenye eneo hilo. Hadi sasa waathirika 740 wako kambini.

Waziri Mkuu ambaye aliwasili Ikwiriri, Rufiji akitokea Mlimba, Morogoro aliwaomba wananchi hao waendelee kutulia kwani serikali iko nao na itaendelea kuwahudumia hadi hali yao irejee katika hali ya kawaida.



"Naomba mpokee salamu za pole kutoka kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunatambua kuna watu wamepoteza mali na wengine mifugo," amesema.

Amewataka watendaji wa vijiji waendelee kubaini maeneo mapya ya kuishi ambayo yatatumika kuhamisha kaya zilizoathirika. "Watendaji wa vijiji tuainishe maeneo mapya ya kwenye miinuko ili baadaye watu waweze kuhamishiwa huko," amesema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ameziagiza TARURA, TANROADS na TAZARA zishirikiane kufanya ukarabati katika maeneo yote yaliyopata athari wakati Serikali inasubiri kumalizika kwa mvua ili iweze kufanya ukarabati mkubwa.

# Serikali yawashika mkono waathirika wa mafuriko kata ya mhoro



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama amewahakikishia waathirika wa Mafuriko Wilayani Rufiji Mkoani Pwani kuwa Serikali itagharamia huduma zote za msingi zinapatikana wakati wa kipindi hiki.

Ameyasema hayo wakati alipoongoza timu ya Mawaziri watano wa kisekta waliofika kushuhudia athari zilizotokana na Mafuriko katika eneo la Muhoro wilaya ya Rufiji Mkoani Pwani ambapo pia ametoa tahadhali kwa Wananchi katika maeneo yao kuhakikisha wanafuata maelekezo ya Wataalam na viongozi ili kuepukana na athari zitakazoweza kutokea wakati wa mvua zinapoendelea.

Waziri Mhagama amesema timu hiyo imefika katika eneo hilo ili kila Waziri kuhakikisha eneo lake linasimamiwa ipasavyo kwa kutafuta mbinu mbadala za kuhakikisha waathirika hao wanapata huduma zinazostahili.



Aidha waziri Mhagama ametoa wito kwa uongozi wa wilaya ya Rufiji kuhakikisha chakula pamoja na mahitaji yanayopelekwa katika eneo hilo yatumike kwa walengwa na si vinginevyo.

"Kwenye huduma hizi za msingi ni pamoja na chakula, na leo mmeondoka kwenye nyumba zenu na kitu kidogo cha kuwasaidia siku mbili tatu, mmemsikia Naibu waziri wa kilimo hapa tumeshaamua kwamba ni lazima chakula kiletwe cha kutosha na chakula kingine kiko njiani kitaingia leo na kesho, wito wangu mwingine ni kwa viongozi wa wilaya , chakula hiki kigaiwe kwa wahusika tu na si kunufaisha watu wengine ambao hawahusiki ,nitafuatilia na kuhakimisha kinawafikia waathirika." Alisema Mhagama.

# Waziri Mhagama “Awataka wananchi kuondoka maeneo hatarishi”




Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama amewataka wananchi kuondoka katika maeneo hatarishi ili kujikinga na mafurikio ya mvua za vuli zinazoendelea kunyesha.

Kauli hiyo ameitoa wakati alipotembelea na kujionea maeneo yaliyokubwa na mafuriko ya mvua katika Halmashauri ya ya Mlimba Mkoani Morogroro ambapo amewaomba wananchi kuendelea kufuatilia na kusikiliza ushauri wa serikali.

Niwaombe wananchi tuendelee kushikamana ili kupambana na majanga ya Mvua na Mafuriko, ambayo yameleta kadhia kubwa sana kwa wananchi.

"Serikali imetengeneza Mpango wa Dharura wa kukabiliana na mvua za El Nino na mvua za Masika, ambapo serikali itafanya kila linalowezekana kuzuia madhara yasitokee na hasa maisha ya watanzania," alisema Waziri Mhagama

Ameongeza kusema mafuriko ya maji yamesababisha udongo kumomonyoka na kuharibu miundo mbinu ya reli na kuleta madhara mengine mengi niwaombe wanamlimba tuendelee kuangalia na kusikiliza ushauri wa serikali.

"Serikali itaendelea kuhakikisha inapambana dhidi ya magonjwa ya Mlipuko na uhaba wa chakula na madhara mengine ambayo yameathiri wananchi, serikali itakuwa pamoja na nyinyi katika kutatua kadhia hizo alibainisha," Waziri Mhagama

Niwaombe wananchi tuendelee kumuomba wenyezi Mungu hali iliyopo mbele yetu iweze kupita kwa haraka na ipite kwa usalama mkubwa.

Ameeleza kwamba katika utabiri wa hali ya hewa unaoendelea kutolewa unaonesha mvua hizi zinaendelea kunyesha hivyo ni vyema tukaendelea kujichukulia tahadhari sisi wenyewe.



## Naibu Waziri Nderiananga aongoza dua ya kumuombea Rais Samia



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Ummy Nderiananga ameongoza dua ya kumuombea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pia ameungana na Viongozi wa Dini na wananchi kupata Iftar ya pamoja.

Akizungumza mara baada ya dua hiyo iliyofanyika jana katika Kituo cha kulea watoto yatima watoto yatima cha Rahmaan kilichopo Chang'ombe Jijini Dodoma, Mhe. Nderiananga amesema kuwa uamuzi huo wa kufanya dua ya kumuombea Rais Samia ni kwa sababu ya mambo mengi aliyoyafanya katika sekta mbalimbali zikiwemo elimu, maji, afya na miundombinu.

Aidha, Mhe. Nderiananga amewasihi Watanzania kuendelea kudumisha amani na utulivu


ili Taifa liendelee kuwa katika hali ya amani na usalama.

"Tumeamua kufanya dua hii maalum ya kumuombea Mhe. Rais na viongozi wetu wa Serikali pamoja na wazazi wangu". Amesema Mhe. Nderiananga.

Ameongeza "Tunashukuru sana uongozi wa kituo hiki kwa dua nzuri kwa watoto na malezi mazuri ya hawa watoto wetu naamini wamejisikia vizuri na kufurahi tulivyowatembelea leo".

Naye, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amewashauri watoto hao wasome kwa bidii ili kutimiza ndoto zao huku akiwataka kuepuka kujiingiza katika makundi mabaya yatakayosababisha kutotimiza malengo yao.

Mkurugenzi wa Kituo hicho Bi. Rukia Hamis Abdallah ameeleza kwamba kituo hicho kinachohudumia watoto 120 kilianzishwa kwa lengo la kujiendeleza kielimu katika maadili mema ya dini, kusaidia watoto pamoja na watu wanaoishi katika mazingira magumu.



# Serikali yaendeleza mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi amesema Serikali inaendelea na Mipango yake ya kupanga mikakati ya namna ya kupambana na ugonjwa wa Malaria na Mbu wanaoeneza Ugonjwa huo.

Akiongea katika kikao cha ngazi ya Makatibu Wakuu wa Wizara kilichohusu ushirikiano wa Kisekta, katika Mapambano dhidi ya Malaria kilichofanyia mapema Jijini Dodoma katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Dkt. Yonazi alisema lengo la kikao hicho ni kuhakikisha Serikali inatengeneza mfumo mzuri wa namna ya kupambana na malaria nchini ili kuweza kuokoa nguvu kazi

Taifa la Tanzania na rasilimali zitakazotumika katika kutibu ugongwa huo.

"Tunaamini kwamba tunapokuwa na Taifa ambalo halina Malaria tunaweza kuongeza Tija katika uchumi na katika maendeleo kwa haraka katika Nchi yetu kwa hivyo nitoe wito kwa Makatibu Wakuu na wadau wote tunaoshirikiana kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvu ili tuweze kupambana na ugonjwa wa Malaria na vilevile mbu waenezao ugonjwa huo." Alisisitiza Dkt. Yonazi

Aidha Katibu Mkuu Yonazi Alitoa wito kwa Jamii ya Watanzania kuendelea kushirikiana na Serikali na Wadau mbalimbali ili kuhakikisha, jamii hizo zinapambana na Mbu waenezao Malaria katika Nyumba zao na mazingira yanayowazunguka.



Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz